## Orodha ya Usikilizaji na Mazungumzo kwa…

### Kuzaliwa hadi miezi 3

- ☐ Kutulia kwa sauti alizozoea au sauti zingine
- ☐ Je anashtuka au kuruka wakati tuna sauti za ghafla

### Miezi 3 hadi 6

- ☐ Kugeuza kichwa au macho kuelekea sauti ya kuvutia
- ☐ Anajisikia kusikiliza
- ☐ Anaweza kuamka kwa sauti kiurahisi
- ☐ Anaanza kusema maneno-kama sauti

### Miezi 6 hadi 12

- ☐ Kuelewa maneno rahisi, k.m. 'Hapana' & 'kwa heri'
- ☐ Kuanza kuiga maneno sauti
- ☐ Inageuza kichwa kwa sauti rahisi

### Miezi 12 hadi 18

- ☐ Kuonekana kuelewa maneno zaidi kila wiki
- ☐ Wakati akiulizwa, anaelezea watu, sehemu za mwili au midoli
- ☐ Anafuata maelekezo rahisi yanayotolewa k.m. 'Kaa chini'
- ☐ Anasema maneno mawili au matatu ya kweli k.v. "mpira', "mbwa" , "gari"

**Ikiwa una wasiwasi juu ya kusikia kwa mtoto wako, unaweza kumwita daktari wako wa kusikia au mfanyakazi wa Kliniki ya mahali.**

Reviewed 2018





**Programu ya Kusikia ya Afya ya Queensland inalenga kutambua watoto waliozaliwa na tatizo la kudumu la Kusikia. Ni bure na inapatikana kwa watoto wote wanaostahili kwa Medicare na waliozaliwa huko Queensland.**

**www.health.qld.gov.au/healthyhearing**

Queensland Government

Language: Swahili



# Utajuaje kama *ninaweza* kusikia?

## Kipimo cha kusikia mtoto wako

Queensland Government

# Kipimo cha kusikia mtoto wako

Kusikia kwa afya ni muhimu kwa kuweza kusema kwa mtoto wako na maendeleo ya lugha tangu miezi ya mwanzo ya maisha. Karibia mtoto mmoja au wawili kati ya kila 1000 watakuwa na tatizo kubwa la kusikia.

Ikiwa tatizo la kusikia halitachukuliwa hatua za mwanzo, inaweza kuathiri kusema kwa mtoto wako na maendeleo ya lugha na kujifunza baadaye shuleni.

## Miadi ya kipimo cha

…………………………..

Tarehe…………………..

Mda ……………………..

Mahali …………………..

### Sehemu ya uchunguzi ya afya ya mtoto

Mpango wa Usikilizaji wa Afya unalenga kutambua watoto waliozaliwa na tatizo la kusikia la kudumu. Ni bure na inapatikana kwa watoto wote waliozaliwa Queensland ambao wanastahili Medicare.

Mtoto wako atapewa idadi ya vipimo vya afya baada ya kuzaliwa. Moja ya haya itakuwa kipimo cha tatizo la kusikia. Kipimo hiki kinapaswa kufanyika haraka iwezekanavyo baada ya kuzaliwa. Ikiwa kipimo hakifanyiki kabla ya wewe na mtoto wako kuondoka Hospitali, mtoto wako anaweza bado kufanyiwa kipimo kama mgonjwa baada ya kwenda nyumbani.

### Jinsi gani kipimo kinafanyika?

Kipimo cha kusikia hakiumizi mtoto wako. Muuguzi au mtu aliyefunzwa katika uchunguzi wa kusikia atafanya kipimo wakati mtoto wako ametulia au amelala. Vitambaa vidogo vilivyowekwa kwa upole juu ya kichwa cha mtoto wako na kipaza sauti kidogo kitawekwa juu ya kila sikio. Mfululizo wa sauti laini utaweza kucheza kwenye masikio ya mtoto wako. Vitambaa vitaandika majibu ya mtoto wako kwa sauti.

### Nitajua lini matokeo?

Matokeo ya kipimo yatajulikana mara moja, na yataandikwa katika Rekodi ya Afya ya Bin-afsi ya mtoto wako. Mtu anayefanya kipimo atajadili matokeo na wewe. Uliza maswali ikiwa kuna kitu ambacho hujui.

### Ni habari gani ambayo kipimo kitatupa?

Kwa kila sikio, kipimo kitawapa matokeo ya 'kupitisha' au matokeo ya 'kurejesha'. Kipimo hakitatoa maelezo ya kina kuhusu kusikia kwa mtoto wako.

### Matokeo ya 'kupita' yanamaanisha nini?

Matokeo ya 'kupita' kwa masikio yote mawili yanaonyesha kwamba hakuna uwezekano wa mtoto wako kuwa na tatizo la kusikia ambalo litaathiri kusema kwao na maendeleo ya lugha.

Idadi ndogo ya watoto wanaweza kupita kipimo, lakini wakawa na aina ya hatari za tatizo la kusikia ambazo huchukua muda mrefu ili kuonekana. Ikiwa hiyo ndivyo ilivyo, mtoto wako atapewa kipimo cha kusikia na dakatri wa kusikia wakati mwingine kabla ya siku yao ya kuzaliwa ya kwanza. Muda wa kipimo huu utategemea mahitaji ya mtoto wako. Wakati ni watoto machache sana wenye sababu hizi za hatari watakuwa na tatizo hili la kusikia, ni muhimu kuhakikisha mtoto wako anapata kipimo chake.

Kumbuka kwamba kusikia kwa watoto wachanga wote na watoto kunaweza kubadilika kwa muda. Ikiwa wakati wowote una wasiwasi kuhusu kusikia kwa mtoto wako mchanga au mtoto, wasiliana na daktari wako au wafanyakazi kwenye kliniki yako ya ndani. Vipimo vya kusikia vinaweza kufanywa kwa watoto wachanga na watoto wa umri wowote.

### Matokeo ya 'kurejesha' yanamaanisha nini?

Matokeo ya 'kurejesha' juu ya kipimo cha kusikia yanaweza kusababishwa na mambo kadhaa:

- mtoto wako hakuwa ametulia wakati wa kipimo
- kunaweza kuwa kulikuwa na kelele za nyuma wakati wa kipimo
- mtoto wako anaweza kuwa na mafua au vizuizi vya muda mfupi katika sikio baada ya kuzaliwa
- idadi ndogo ya watoto wanaweza kuwa na matatizo ya kusikia ya muda mfupi au ya kudumu. Kiwango cha kupoteza kinaweza kutofautiana kutoka kwa kawaida hadi kubwa zaidi.

Ikiwa kipimo chako cha kwanza cha mtoto cha kusikia kinaonyesha matokeo ya 'kurejesha' kwenye mojawapo ya sikio moja au yote, kipimo cha pili cha kusikia kwenye masikio yote kitafanywa.

Ikiwa kipimo chako cha pili cha kusikia cha mtoto kinaonyesha matokeo ya 'kurejesha' kwenye mojawapo ya sikio au yote, utaelekezwa kwa Daktari wa kusikia kwa ajili ya kupima na huduma ya msaada wa familia. Utapewa brosha ya ziada inayoelezea hili kwa undani zaidi.

### Ni wapi naweza kupata maelezo zaidi?

Ikiwa ungependa habari zaidi kuhusu kipimo cha kusikia cha mtoto wako, wasiliana na hospitali yako ya mahali, daktari wa mtoto wako, au wafanyakazi katika kliniki yako ya mahali.



